

MKATABA WA PANGO

Mkataba huu umefanyika leo tarehe 12 Mwezi 10 2023.

BAINA YA

EWALD IZACK CHUWA wa S. L. P 36009, Dar es Salaam, ambaye kwa upande wa kwanza ataitwa ("MPANGISHAJI"), kwa masharti ya mkataba huu hilo neno litawahusisha warithi na wawakilishi wake wa kisheria na mtu mwingine yeyote aliye chini yake.

NA

SALAMA FABRIQUE LIMITED wa S. L. P....., Dar es salaam , ambaye kwa upande wa pili wa mkataba huu ataitwa ("MPANGAJI"), kwa masharti ya mkataba huu hilo neno litawahusisha warithi na wawakilishi wake wa kisheria na mtu mwingine yeyote aliye chini yake.

Kwamba **EWALD IZACK CHUWA** ni Mmiliki halali wa Nyumba, iliyopo katika **Kiwanja No. 2,3 & 4, Kitalu K, Eneo la Kisarawe II, Manispaa ya Kigamboni, Dar es Salaam**. Kwa mkataba huu Mpangishaji ameamua kumpangisha Mpangaji **GODOWN** katika nyumba husika kwa ajili ya biashara

HIVYO basi mkataba huu unashuhudia yafuatayo:

1. Kwamba, mkataba huu husika ni wa muda wa **Miaka Mitatu (03)** kuanzia tarehe **18/12/2023** mpaka tarehe **18/12/2026**.
2. Kwamba, Mpangishaji na Mpangaji wote kwa pamoja wamekubaliana kuwa Mpangaji atakuwa akihuisha Mkataba huu wa Pango kila baada ya **Mwaka Mmoja (01)**.
3. Kwamba, Kodi ya Godown hiyo itakua ni **fedha za kitanzania Shilingi Milioni Tisini (TZS 90,000,000/=)** tu kwa kipindi chote cha **Miaka Mitatu (03)**, ambayo ni sawa na Fedha za Kitanzania **Shilingi Milioni Thelathini (TZS 30,000,000/=)** tu kwa kila Mwaka, na kwa kila mwezi kodi hiyo ni sawa na kiasi cha fedha za Kitanzania Shilingi **Milioni Mbili na Laki Tano (TZS 2,500,000/=)**
4. Kwamba Mpangaji na Mpangishaji wamekubaliana kwamba kodi tajwa hapo juu itakuwa inalipwa kwa mwaka ambayo ni **jumla ya kiasi cha fedha za Kitanzania Shilingi Milioni Thelathini (TZS 30,000,000/=)** tu.



5. Mpangaji atalipia malipo hayo ya Mwaka Mmoja (01) tajwa hapo juu siku ya kusaini Mkataba huu.
6. Mpangishaji atakuwa na uwezo wa kupanga bei upya au kubadili masharti ya mkataba kila mkataba mpya unaposainiwa.
7. Kodi zote za serikali pamoja na gharama za **Ulinzi, Usafi, Maji na Umeme** zitamhusu Mpangaji.
8. Kwamba Mpangishaji hatakiwi kupangisha pango husika kwa mpangaji mwingine bila kibali cha mwenye nyumba.
9. Kwamba Mpangishaji anaweza kuvunja mkataba huu kwa kutoa taarifa mwezi Mmoja ila Mpangishaji atatakiwa kurudisha kodi ya miezi ambayo mpangaji hajaitumia.
10. Kwamba wakati mkataba huu utakapofika ukomo wake Mpangaji anatakiwa kurudisha godown husika kwa Mpangishaji ikiwa katika hali nzuri kama ilivyokuwa wakati anakabidhiwa
11. Kwamba Mpangishaji ataruhusiwa kuingia na kukagua sehemu ya pango husika pale inapobidi na Taarifa ya awali itatolewa kwa Mpangaji endapo kutakuwa na uharibifu wowote uliofanyika Mpangaji atawajibika kufanya marekebisho.
12. Mkataba huu unaongozwa na Sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; endapo upande wowote katika Mkataba huu utavunja au kukiuka masharti ya Mkataba huu Sheria itachukua Mkondo wake.

IMEKUBALIWA NA KUWEKWA SAHIHI na
EWALD IZACK CHUWA
ambaye namfahamu/ametambulishwa kwangu na

Tarehe...18...mwezi...12...2023

MBELE YANGU:-

Jina;.....DOMINA MNDASHA.....

Sahihi.....[Signature].....

Anuani.....S.I.P 32517 DSA.....

Wadhifa.....WAKILI.....

[Signature]
MPANGISHAJI



IMEKUBALIWA NA KUWEKWA SAHIHI na
HE BAIQUAN kwa niaba ya
SALAMA FABRIQUE LIMITED
ambaye namfahamu/ametambulishwa kwangu na

Tarehe...18...mwezi...12.....2023


MPANGAJI

SHAHIDI WA MPANGAJI

Jina: HE YUAN.

Sahihi... 

Anuani... 21091

Uhusiano:

MBELE YANGU:-

Jina: DOMINA MNDASHA

Sahihi... 


Anuani... S-L-P 32512 DSM

Wadhifa... WAKU



STAMP DUTY

TShs: 300,000/= Collected
9934114280991 Date: 21/12/2023


Kigamboni Tax Service Centre